# Kuchunguza
## Maandiko Matakatifu

**Emmaus Shule ya Biblia**
**Kwa Njia ya Posta**

## *SOMO LA KWANZA*
## *MAFUNDISHO YA MAANDIKO MATAKATIFU KUHUSU MAANDIKO YENYEWE.*

## *UTANGULIZI:*

Biblia nzima huitwa "Maandiko Matakatifu", yaani Neno la Mungu pekee linalotoa habari za Mungu kwa ulimwengu. Tunasoma kwamba "Maandiko Matakatifu yote ni pumzi ya Mungu" (2 Timotheo 3:16). Maana yake ni kwamba Mungu aliwaongoza watu ambao waliyaandika.

Maandiko Matakatifu yameandikwa katika vitabu 66. Vitabu 39 ni Agano la Kale, na 27 ni Agano Jipya. Bwana Yesu Kristo alisema:

"Maandiko (Matakatifu) hayawezi kutanguka," (Yohana 10:35) kwa hiyo tuyafuate kwa moyo wote yaliyoandikwa kama alivyofanya Yeye. Biblia ni kitabu chenye ukweli, miujiza, unabii na mashairi; tena ni kitabu chenye maadili na mafundisho ya kiroho. Watu wengi, tangu zamani na mpaka leo, wameichukia Biblia na kujaribu kuiharibu, lakini wameshindwa kwa sababu "Neno la Bwana hudumu hata milele" (1 Petro 1:25).

## *AGANO LA KALE:*

Kitabu cha "Mwanzo", ambacho ndicho cha kwanza katika Biblia, hutufunulia mwanzo wa vitu vyote, isipokuwa mwanzo wa Mungu peke yake, ambaye hana mwanzo wala mwisho. Mwanzo wa ulimwengu, maisha, watu, dhambi, wokovu, ndoa, jumuiya, mataifa, mashairi, nyimbo, maarifa, na mwanzo wa kila kitu tukijuacho, umefunuliwa katika kitabu hiki cha ajabu. Vitabu 16 vinavyofuata, kuanzia kitabu cha "Kutoka" mpaka "Esta", hueleza kikamilifu juu ya Waisraeli. Vitabu 5 kuanzia "Ayubu" mpaka "Wimbo Ulio Bora" vimejaa mashairi na nyimbo. Vitabu 17 vinavyobakia tangu "Isaya" mpaka "Malaki" vimejaa habari za Mungu kwa Waisraeli; na unabii wa nyakati zijazo. Agano la kale huungana na Agano Jipya katika kutimizwa kwa unabii huo.

## *AGANO JIPYA:*

Agano Jipya limegawanyika katika sehemu kuu nne: "Injili", "Matendo ya Mitume", "Nyaraka" ishirini na moja, na "Ufunuo". Injili nne hueleza habari za maisha, kufa, kufufuka na kupaa kwake Mwana wa Mungu, Yesu Kristo. Matendo ya Mitume hueleza habari za Wakristo wa kwanza. Nyaraka hutoa mafundisho kwa shuhuda za maisha ya Kikristo, na Ufunuo hutupatia upeo wa mambo yatakayotokea ulimwenguni, mbinguni na katika jehanum kwa nyakati zijazo.

## *MWISHO:*

Biblia ni "taa ya miguu yetu na mwanga wa njia zetu." (Zaburi 119:105) Biblia ni "kama nyundo ivunjayo mawe vipande vipande" (Yeremia 23:29). Ni "neno lenye uzima". (1 Petro 1:23) na "upanga ukatao kuwili" (Waebrania 4:12). Kwa hiyo tuipokee na kuiamini kuwa ni Neno la Mungu pekee na tujifunze neno hilo kwa ajili ya maisha yetu.

## *SOMO LA PILI*

### Mafundisho ya Maandiko Matakatifu kuhusu Mungu (1)

Maandiko Matakatifu huhakikisha kuwepo kwa Mungu. Yeye hana mwanzo wala mwisho, ni Mkuu kupita wote, na Muumba wa ulimwengu. "Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi" (Mwanzo 1:1). Mungu ni mwenye elimu yote, mwenye nguvu zote, yupo mahali pote, mbinguni na duniani. Tena maandiko hutufundisha kuwa Mungu ni Mtakatifu (1 Petro 1:15-16) na mwenye Upendo (1 Yohana 4:8), tena ni Mwaminifu kabisa (1 Wakorintho 10:13). Amri aliyompa mwanadamu ni hii: "Usiwe na miungu mingine ila Mimi", (Kutoka 20:3). Mungu peke yake anastahili kuabudiwa, kuheshimiwa na kutumikiwa.

## *UTATU WA MUNGU:*

Mungu ni mmoja tu (1 Timotheo 2:5). Ingawa ni mmoja, tunafundishwa kuwa ana nafsi tatu: Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Katika Mathayo 28:19, nafsi hizi tatu za Mungu zimetajwa badala ya jina moja. Sehemu nyingine hufundisha juu ya utatu huo.

Katika Mathayo 3:16-17 tunasoma hivi:

"Naye Yesu alipokwisha kubatizwa, mara aliibuka kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, na kutua juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikasema: Huyu ni Mwanangu, Mpendwa wangu, ninayependezwa naye."

Hapa Utatu wa Mungu unaonekana, na kila nafsi ina kazi yake.

## *MUNGU BABA:*

Mstari katika Biblia unaotueleza kuwa Mungu Baba ni Mungu kweli, ni Warumi 1:7: "Neema na iwe kwenu na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo." Yeye ni Roho (Yohana 4:24) naye hutajwa wa kwanza katika Utatu. Lakini Utatu wote una nguvu sawa, kila nafsi ina nguvu na uweza sawa na nyingine pasipo kuzidiana. Sehemu nyingi za Biblia husema kwamba yeye ni Baba.

Mfano: Neno la Bwana Yesu katika Mathayo 6:9. "Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe." Anao mpango kwa ulimwengu wote, pamoja na wanadamu wote, naye amejidhihirisha kwetu. Musa, kiongozi mmojawapo mashuhuri wa taifa la Israeli, alimwomba hivi:

"Ee Bwana Mungu, umeanza kumwonesha mtumishi wako ukubwa wako, na mkono wako wa nguvu; kwani kuna Mungu gani mbinguni au duniani awezaye kufanya mfano wa kazi zako, na mfano wa matendo yako yenye nguvu?"(Kumbukumbu la Torati 3:24).

Yeye ni Mungu wa upendo, neema, huruma, fadhili, utakatifu, yuko hai, na ni mtoaji wa mema yote. Kwa upendo wake mkuu, alimtoa Mwanawe Yesu Kristo. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." (Yohana 3:16).

***Je, umewahi kumshukuru Mungu kwa kumtoa Mwanawe ili aje akuokoe katika dhambi zako?***

## *SOMO LA TATU*

**Mafundisho ya Maandiko Matakatifu kuhusu Mungu (2)**

## *MWANA WA MUNGU*

Bwana Yesu Kristo ni Mungu Mwana. Yeye naye hana mwanzo bali ni wa milele. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno (Kristo), naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." (Yohana 1:1). Mtu yeyote asije akafanya kosa kubwa kwa kusema kwamba Yesu hakuwako au siyo Mungu! Anaitwa "Imanueli - Mungu pamoja nasi" (Mathayo 1:23). "Kristo ni Bwana" (Luka 2:11), "ni Neno" (Yohana 1:1). Katika Waebrania 1:8 tunasoma, "Kiti chako cha enzi, Ee Mungu, ni cha milele."

Vile vile Kristo si Mungu tu, bali pia alikuwa mwanadamu. Aliacha raha za mbinguni, akaja ulimwenguni, akazaliwa na bikira Mariamu. Akaitwa Yesu, maana yake: "Wokovu wa Mungu" (Mathayo 1:21).

Alikuwa Mungu aliyedhihirika katika hali ya mwanadamu (1 Timotheo 3:16). Sawa sawa na wanadanu wengine, aliona uchovu na njaa, lakini hakufanana na sisi kwa kutenda dhambi. Neno la Mungu lasema: "Yeye hakutenda dhambi," (1 Petro 2:22). Alikuja ili aweze kuwa mkombozi wa ulimwengu. "Katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi ndiye Kristo Bwana." (Luka 2:11). Alizaliwa Bethlehemu, akaishi Nazareti. Kwa muda wa miaka mitatu na nusu, aliwahubiria watu, akaponya wagonjwa, akawatayarisha wanafunzi wake kwa kazi ya siku za mbele. Habari kuu katika Biblia inahusu kufa na kufufuka kwake Yesu Kristo. Watu wabaya walimshtaki bila kosa, wakampeleka kwa Pilato. Akahukumiwa kifo cha msalaba, akasulubiwa huko Golgotha nje ya mji wa Yerusalemu; akiwa katikati ya wevi wawili.

"Lakini," unaweza kuuliza, "kwa nini alikufa iwapo hakukosa wala kutenda dhambi?"

Sehemu nyingi katika Biblia hujibu swali hilo.

Isaya 53:5-6: "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote."

Warumi 5:8: "Bali Mungu aonesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi." 1 Wakorintho 15:3: "Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kama yanenavyo maandiko." Hivyo alikufa ili wewe na mimi tupate wokovu. Tutajifunza juu ya jambo hilo katika somo la 5. Siku ya tatu baada ya kusulubiwa, alifufuka kutoka katika wafu (1 Wakorintho 15:4)! Baadaye aliwatokea mitume na watu wengine kabla ya kupaa kwake kwenda mbinguni, na kukaa mkono wa kuume wa Mungu Baba. (1 Wakorintho 15:6; Matendo 1:9). Siku moja atarudi tena! (Matendo 1:11; 1 Wakorintho 15:23; 1 Wathesalonike 4:16).

## *ROHO MTAKATIFU:*

Roho Mtakatifu ni Mungu. Tunasoma haya katika Matendo ya Mitume 5:3,4. Roho naye ni nafsi ya Mungu, si kishawishi kama wengine waaminivyo na kufundisha. Kazi yake mojawapo ni kuuonya ulimwengu juu ya dhambi, utakaso na hukumu; (Yohana 16:8). Ni msaidizi (Yohana 14:16,17,26), ni kiongozi (Yohana 16:13), hufundisha (Yohana 14:26), naye huweza kuhuzunishwa (Waefeso 4:30) na kuzuiwa kufanya kazi ndani yetu. Roho ni nafsi ya Mungu aliyewaongoza wanadamu wakati walipoandika maandiko ya Biblia. (2 Timotheo 3:15,16; 2 Petro 1:21). Naye hukaa ndani ya waamini, kama tunavyosoma katika 1 Wakorintho 3:16, Huwajaza nguvu ili waishi katika hali ya kumpendeza Mungu.

## *SOMO LA NNE*

**Mafundisho ya Maandiko Matakatifu kuhusu Mwanadamu**

## *KUUMBWA KWA MWANADAMU:*

Mungu ndiye aliyeumba mbingu na nchi, jua, mwezi, na nyota. Akaumba pia samaki, ndege wa angani, wanyama, na mimea. Kisha, Mungu akamwumba mwanadamu. Tunasoma katika kitabu cha Mwanzo 1:27. Adamu ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza, na kisha Hawa akaumbwa ili awe mke wake. Lo! huu ni uumbaji wa ajabu! Wanadamu waliumbwa ili wamtukuze Mungu. Hata sisi tunatakiwa tuwe hivyo. Mungu anatutaka tumpende na kumtumikia Yeye, ili tuweze kuishi katika furaha pamoja naye.

## *ANGUKO LA MWANADAMU:*

Adamu na Hawa waliishi pamoja na Mungu siku zote, lakini siku moja Hawa na Adamu walikosa kumtii Mungu; nao wakatenda dhambi (Warumi 5:12). Hivyo baadaye walikufa kwa sababu ya dhambi. Kwa tukio hilo, mwanadamu huzaliwa katika asili ya dhambi. Wote tumetenda dhambi. Katika kitabu cha Warumi 3:23 tunasoma, "Wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Jambo hili linaonesha kwamba tumeshindwa kufikia lengo la kukamilika kadiri Mungu alivyotutaka. Mawazo mabaya na matendo mabaya ni dhambi machoni pa Mungu. Maandiko yanasema: "Hakuna mwenye haki hata mmoja," (Warumi 3:10). Kwa hiyo wewe na mimi tujue hakika kwamba tumefanya dhambi kwa mawazo, maneno na matendo. Tunatakiwa kukubali mbele za Mungu kwamba tumefanya dhambi. Biblia inasema: "Tukisema kwamba hatuna dhambi, tunajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu." (1 Yohana 1:8).

## *HUKUMU YA MUNGU KWA MWANADAMU:*

Si Neno la Mungu tu linaloonesha dhambi, bali hata ule utakatifu wa Mungu hupingana na dhambi katika maisha yetu. Mungu ni Mtakatifu, hivyo hawezi kushiriki katika uchafu wa dhambi. Tena Yeye ni Mungu wa haki, hivyo ametoa hukumu kwao watendao dhambi. Maandiko yanasema, "Mshahara wa dhambi ni mauti," (Warumi 6:23). "Mauti hiyo" ni kule kutengwa na Mungu kiroho. Hata dhambi imeleta kifo cha kimwili kwa mwanadamu, ndiyo maana watu huishi kwa miaka fulani, kisha wanakufa. Katika Waebrania 9:27 tunasoma:

"Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu."

Hukumu ya mwisho kwa watu wote wasiookoka ni jehanum, ziwa la moto uwakao. Imeandikwa katika Ufunuo 20:15 kuwa "Na iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto." Hukumu hiyo ya kutisha itakuwa ya milele, ambayo unahitaji kujiepusha nayo. Je, unapenda kwenda jehanum katika ziwa lile la moto?

## *SOMO LA TANO*

### Mafundisho ya Maandiko Matakatifu kuhusu Wokovu

Watu huuliza maswali mengi sana kuhusu wokovu. Katika somo hili tutajifunza juu ya maswali matatu:

1.Wokovu ni nini?

2. Jinsi gani mtu anaweza kuokoka?

3. Ni mtu gani anayeweza kuokoka?

## *1. WOKOVU NI NINL?*

Wokovu ni ukombozi. Biblia hueleza ukombozi huo kitaifa, kimwili na kiroho. Kitaifa: Waisraeli waliokolewa kutoka katika utumwa huko Misri (Kutoka 13:14). Hawakuweza kujiokoa wenyewe, mpaka Mungu mwenyewe alipowakomboa na kuwatoa Misri. Kimwili: Danieli aliokolewa na Mungu, hata asidhurike na simba katika pango (Danieli 6:22-23). Lililo kubwa zaidi kuliko njia hizo mbili ni "wokovu wa kiroho". Kwa roho, wanawake na wanaume waliolemewa na dhambi na kungojea hukumu, wanaweza kupata wokovu huo mkuu; lakini kwa nafsi zao hawawezi kujiokoa, bali ni kipawa cha Mungu mwenyewe. Zaidi ya yote wokovu huo, haupatikani kutoka kwenye kanisa fulani, katika ubatizo au kwa mtu fulani, bali hupatikana kwa Bwana Yesu Kristo.

> "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu." (Waefeso 2:8-9).

Kwa njia ya wokovu huo mkuu, huja furaha ya kusamehewa, nguvu ya kuishi maisha ya kikristo, na matumaini kuwa siku moja tutanyakuliwa juu mbinguni na kuishi pamoja na Mwokozi wetu, milele na milele.

## *2. JINSI GANI MTU ANAWEZA KUOKOKA ?*

Wokovu hupatikana kwa njia ya Yesu Kristo tu. Biblia inasema: "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." (Matendo 4:12). Ili kuokoka ni lazima utubu dhambi zako kabisa kwa Yesu, na kwa imani umpokee Kristo Yesu kuwa Mwokozi na Bwana wako. "Bali wote waliompokea (Yesu) aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake," (Yohana 1:12). Maandiko yanasema: "Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka." (Matendo 16:31).

## *3. NI MTU GANI ANAYEWEZA KUOKOKA?*

Wewe na mimi tunaweza kuokoka. Wokovu ni kwa kila mtu, haubagui taifa, kabila, lugha, asili ya mtu, elimu au utamaduni. "Injili, yaani habari njema, ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye." (Warunu 1:16). Ikiwa hata wewe unaweza kuokoka, kwa nini usimpokee Kristo kuwa Mwokozi wako tangu sasa? Mwendee uombe hivi: "Bwana Yesu, ninakiri kuwa mimi ni mwenye dhambi, na ninasikitika kwa dhambi zangu. Ninashukuru kwa kunifia msalabani ili nipate wokovu. Sasa najiweka mikononi mwako kwa imani ili uwe Mwokozi wangu." Usichelewe kuchukua hatua hii ya maana katika maisha yako. Huu ndio wakati wa kufanya hivyo. "Wakati uliokubalika ndiyo sasa, siku ya wokovu ndiyo sasa?" (2 Wakorintho 6:2).

## *SOMO LA SITA*

**Mafundisho ya Maandiko Matakatifu kuhusu Kuomba na Kusoma Biblia.**

Kuomba, kusoma Biblia, ushirika katika kanisa, na kushuhudia, ni mambo muhimu kwa Mkristo. Katika masomo haya mawili tutajifunza mambo hayo ili tuishi kwa ajili ya Kristo.

## *KUOMBA:*

Kuomba ni kuzungumza na Mungu. Kwa kawaida maombi ni kwa Mungu Baba, kupitia katika jina la Bwana Yesu Kristo. (Luka 11:2; Yohana 15:16; Waefeso 3:14-21). Katika maandiko, watu wengine walimwomba Bwana Yesu, lakini hatuoni mfano wowote ambapo watu walimwomba Roho Mtakatifu.

Bwana Yesu alimwomba Mungu kila wakati. Tunasoma katika Mathayo 14:23 kuwa "alipanda mlimani faraghani kwenda kuomba". Mtume Paulo naye aliomba; akisema:

"Hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu." (Wakolosai 1:9).

Wewe na mimi pia tunahitaji kuomba. Mwombe Mungu wetu kila asubuhi na jioni, ukijitenga katika sehemu ya pekee chumbani ili uongee na Mungu. Unapoomba, mshukuru Mungu kwa kutupatia Mwokozi, waombee jamaa, marafiki na majirani zako, tena jiombee mwenyewe, ili uishi katika ulinzi wa Mungu. Mwombe akufanye kuwa msaada na baraka kwa watu wengine. Akupe uongozi, nguvu, hekima kila siku na mengine mengi. Usidharau nafasi hii ya kuzungumza na Mungu kwa maombi.

## *KUSOMA BIBLIA:*

Katika somo la kwanza tulijifunza juu ya Biblia. Habari zake zimewabadilisha watu wengi, wanaume, wanawake, vijana na wasichana tangu zamani hata leo. Kusoma na kujifunza Biblia ni hatua mojawapo ya maana katika maisha na kazi ya mkristo. Ni muhimu kukua "katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo."(2 Petro 3:18).

Neno la Mungu hutupatia chakula cha roho. Tusipokula tutakuwa wadhaifu na wanyonge. Bwana Yesu alisema, "Mwayachunguza maandiko" (Yohana 5:39). Waungwana, "Wakayachunguza maandiko kila siku" (Matendo 17:11).

Tunahitaji kutenga muda kila siku kwa ajili ya kujisomea Biblia, na kumwomba Mungu atueleweshe hayo tuliyoyasoma. Kusoma kwa utaratibu pamoja na kuomba ni jambo la muhimu. Soma vitabu vingine vya Kikristo na masomo ya Biblia kwa njia ya Posta ili ujue mengi ya ajabu katika Biblia. Mwalimu mmoja maarufu wa Biblia alitoa wosia huu:

"Jitoe kabisa katika kusoma maandiko, kisha uyaweke moyoni mwako."

## *SOMO LA SABA*

**Mafundisho ya Maandiko Matakatifu kuhusu Ushirika wa Kanisa, Ushuhuda, na Maisha Mapya.**

## *USHIRIKA WA KANISA:*

Wakati tunapompokea Kristo kama Mwokozi wetu, tunakuwa washiriki wa kanisa. Kanisa ni kila mwamini katika Bwana Yesu Kristo, bila kubagua rangi, taifa na utamaduni. (1 Wakorintho 12:12-13). Washiriki wa kanisa wapo ulimwenguni kote, ingawa kanisa hilo halijawahi kukusanyika mahali pamoja. Na mkuu wa kanisa hilo ni Bwana Yesu mwenyewe, hakuna mwingine (Wakolosai 1:18-19). Lakini nafasi ipo kwa wakristo wa kweli wa eneo fulani kukusanyika mahali popote. Kukusanyika kwao kunawafanya washirikiane pamoja

(1 Yohana 1:7) na kumega mkate wakimkumbuka Bwana Yesu kwa ushirika mtakatifu (Matendo 20:7) na kuomba pamoja (Matendo 12:12); kunatoa nafasi ya kusikia Neno la Mungu kutoka katika Maandiko (Matendo 13:1), pia huduma mbalimbali za Kikristo zinaweza kufanyika.

Tunatakiwa kushiriki katika kanisa au kusanyiko la mji au kijiji fulani na kuhudhuria mikutano inayopangwa. Ni jambo jema pia kufanya urafiki na waamini wengine ili tuweze kuimarika katika imani yetu ya Kikristo.

## *KUSHUHUDIA:*

Bwana Yesu kabla ya kupaa kwenda mbinguni aliwaagiza wanafunzi wake kwenda ulimwenguni kote, ili wahubiri Injili kwa kila kiumbe (Mathayo 28:19,20; Marko 16:15). Na mwisho aliwaahidi kuwa wangepata msaidizi: "Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu na katika Uyahudi..., na hata mwisho wa nchi." (Matendo 1:8). Ili maagizo hayo yatimie, wanafunzi walipata mateso na majaribu mengi. Lakini walivumilia, wakahubiri habari njema kila mahali hali wakiona Bwana yu pamoja nao wakijazwa nguvu za Roho Mtakatifu. Katika kitabu cha Matendo ya Mitume tunasoma kwamba wote walioamini walibatizwa, ubatizo huo ukiwa ni ushuhuda kwao.

Wote tuliompokea Kristo kuwa Mwokozi wetu, lazima tumtumikie yeye. Tunaweza kuwashuhudia wengine nyumbani, shuleni, chuoni, na kazini kwetu. Tena tunaweza kugawa maandiko ya Injili na kuwakaribisha watu waje kanisani na kuwashuhudia kwa ajili ya Kristo. Mungu atatupatia nguvu, ujasiri na msaada tukifanya hivyo kwa ajili yake. Kwa hiyo ni juu yetu kuwaombea wote ambao bado hawajampokea Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wao.

## *MAISHA MAPYA:*

Kila Mkristo anayeshuhudia, anadhihirisha kwamba anampenda Yesu Kristo, Mwokozi wake. Bwana Yesu mwenyewe atamwongoza Mkristo huyo katika njia nyingine pia.

Sikia Bwana Yesu anavyosema: "Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye." (Yohana 14:21).

Hapo ndipo maisha ya Mkristo yanapotofautiana na maisha ya watu wengine: Anazitafuta amri za Bwana Yesu na kuzifuata. Aliyeiba asiibe tena, mwenye kutumia uongo asishuhudie uongo tena, aliyekuwa na uchafu, atafute usafi, chuki, choyo, husuda vitoke, na Mkristo atafute amani, awe tayari kusaidia, ampende jirani yake kama nafsi yake mwenyewe - na mengine mengi yanayomsaidia mtu wa Yesu kuishi maisha ya kumpendeza Mungu.

## *MWISHO:*

Ebu jaribu kujiuliza, "Je, mimi ni Mkristo wa kweli?" Kama sivyo, mwamini Bwana Yesu ili upate wokovu leo. Kama tayari, kumbuka, ni jambo muhimu kuomba, kusoma na kujifunza Neno la Mungu, kujiunga na kanisa linalokubali wokovu, kushiriki katika kumshuhudia Bwana Yesu, pamoja na kutenda mema.

EMMAUS Shule ya Biblia kwa Njia ya Posta
S.L.P.1424, Dodoma
Tanzania
ISBN 978-9976-80-001-2